

MWONGOZO PPI

1. Insha ichukue mtindo na muundo wa **hotuba**.

Utangulizi-kutambua watu kicheo, makaribisho

Mwili-maudhui manane

Tamati –kuwashukuru na kiwaaga

Maudhui

- Wajiamini
- Wapate usingizi mzuri
- Wawe watulivu
- Wasome maagizo na maswali
- Wajibu maswali kwa utaratibu baada ya kuyatafakari
- Wazingatie muda na mahitaji ya maswali
- Waandike kwa hati nadhifu
- Wahariri majibu
 - Mwanafunzi awatii walimu wake.
 - Wanafunzi kufanya kazi ya ziada
 - Kudurusu vitabu mbalimbali
 - Waweze kuzingatia silabasi / mtaala
 - Kufuata sheria za shule
 - Kujiunga kwa makundi ya wanafunzi na kusidiana kimasomo
 - Mijadala ya kutosha iandaliwe baina yao
 - Kufanya mazoezi zaidi katika masomo yote
 - Kuamka mapema kuelekea darasani kusoma
 - Kuepuka kelele darasani
 - Kutopoteza muda wa masomo
 - Kushiriki katika michezo
 - Kutotumia dawa za kulevya.

2. Matatizo yanayowakumba wanafunzi shuleni nchini

- Ukosefu wa karo au sare za shule.
 - Migomo ya walimu
- Migogoro na migomo shuleni
- Ndoa za lazima
- Ndoa za mapema
- Utamaduni na mila kama ukeketaji wa wasichana.
- Mikasa ya moto.
- Uavyaji wa mamba

- Kupigwa na baadhi ya walimu
- Mihadarati / madawa ya kulevya.
- Uhusiano wa kimapenzi miongoni mwa wanafunzi
- Uongozi mbaya shuleni

3. Jitihada haiondoi kudura.

Asimulie kisa kinachodhihirisha jinsi mtu fulani alipatwa na janga ambalo alijaribu mbinu nyingi / kadiri ya uwezo wake na wa wenzake kujinusuwa lakini hakufaulu kwani mipango ya Mungu haiwezi kupanguliwa.

4.

Mtahiniwa aandike kisa cha kubuni ambacho kitamalizikia kwa kuoana na dokezo lililotolewa. Hii ni insha ya Mdokezo. Taharuki ijitokeza vilivyo. Lazima mtahiniwa amalizie kwa maneno hayo. Asipomaliza kwa maneno hayo, ataadhibiwa kimtindo. Mtahiniwa atunge kisa kitakachooana na maneno aliyoandikiwa. Mbinu rejeshi itakuwa mwafaka sana kutumiwa.

